TANGAZO LA SERIKALI NA . 410 la tarehe 23/6/2023

SHERIA YA MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI,

(SURA YA 414)

**NOTISI**

(*Imetolewa chini ya kifungu cha 19(4)*)

NOTISI (TAFTISHI KUHUSU KUBADILISHA BEI KIKOMO ILIYOMO KATIKA KANUNI ZA KUKOKOTOA BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA PETROLI YA MWAKA 2022) YA MWAKA 2023

**KWA KUWA**, EWURA imepokea maombi kutoka kwa Kampuni za uwagizaji mafuta nchini ya kufanya mapitio ya bei kikomo na gharama za malipo utoka asilimi 1 kama ilivyowekwa chini ya Kanuni za Kukutoa Bei Kikomo za Bidhaa za Petroli za Mwaka 2022 hadi asilimia 2.5 na Kanuni kuhakikisha kuwa wastani linganifu wa viwango vya kubadilishia fedha vinaakisi uhalisi wa gharama zilizotumika.

**NA KWA KUWA**, EWURA imepewa mamlaka cjhini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kufanya taftishi kwa kadri itakavyoona inafaa kwa ajilii ya utekelezaji bora wa majukumu yake.

**HIVYO BASI**, Notisi ya ufanyikaji taftishi inatolewa kwa umma kama ifuatavyo:

Jina

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi (Taftishi kuhusu Kubadilisha Bei Kikomo Iliyomo katika Kanuni Ndogo za Kukokotoa Bei Kikomo za Bidhaa za Petroli ya Mwaka 2022) ya Mwaka 2023.

Lengo la taftishi

2. Lengo la taftishi ni kuiwezesha Mamlaka kukusanya maoni ya wadau kuhusu marekebisho ya gharama za benki ili kufanya uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na pia kuweka tafsiri halisi ya viwango

vya kubadilishia fedha za kigeni vilivyopo katika masoko ya fedha vinavyotumika katika kukokotoa bei kikomo za mafuta kwa kila mwezi.

Jinsi ya kushiriki kwenye taftishi

3. Mtu yeyote anayetaka kushiriki kwenye taftishi anaweza kufanya hivyo kwa kuwasilisha maoni ya maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu kupitia anwani iliyotajwa katika aya ya 4 ya Notisi hii ndani ya siku tano baada ya tarehe ya Notisi hii.

Anwani ya Mamlaka

4. Anwani ya Mamlaka itakuwa:

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,
Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA,
41104 Tambukareli,
S.L.P. 2857,
Dodoma, Tanzania.

Dodoma,
.........................., 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
*Mkurugenzi Mkuu*